# *Kushawishika Na Kisha Kuhusika*

Asante sana, Ndugu Carl.

2 Mnaweza kuketi. Mambo mengi—mambo mengi sana ya kusemwa, na—na muda unaenda. Lakini hakika nina furaha kuwa hapa, usiku wa leo, Chicago, na kumshukuru Ndugu Carlson, na Ndugu Boze kwa wema wao, na wengine wote, kwa kunialika hapa, usiku wa leo, kuzungumza kwenye chakula hiki cha mchana, ama chakula cha kutwa, kwa kuwa Ndugu yetu Boze anaenda kwenye huduma ya umishenari. Ninajua yale anayopitia kule, kwa sababu mimi pia ni mmishenari, nami nilikuwa nimeketi hapa pamoja na ndugu kutoka Afrika Kusini aliyekuwa katika mikutano yetu kule, tulipokuwa mara ya mwisho Afrika Kusini.

3 Na wakati yule daktari, rafiki wa thamani alipokuja hapa na kuongoza maombi hayo kwa ajili yetu, na jinsi ambavyo sisi sote tunajua jinsi hisia za msituni zilivyo wanapoingia mle, nami nafikiri ni jambo linalostahili. Mnajua, ninii, kwamba tuna makanisa kwenye kila kona, na kuisikia Injili kwa njia yoyote tunayotaka kuisikia, hao watu kule hawajawahi kusikia Jina la Yesu, mara nyingi.

4 Kwa hiyo ninajiandaa kurudi tena. Sijawahi kuridhika nyumbani, nami siamini ninaweza kuridhika mpaka nitakaporudi hudumani tena kule. Na kwa hiyo, niombeeni. Na kuhusu milango kufungwa kwangu, ninatarajia jambo hilo, kwa hiyo ninaninii tu. . .Asanteni. Mkiendelea kuniombea, ombeni tu kwamba nitaninii—kwamba nitadumu katika mapenzi ya Mungu, hilo ndilo jambo muhimu.

5 Na sasa, na mwaombee ndugu pia. Hilo ni sawa, kama hawalioni, mbona. . .Afadhali nigeuke upande huu *hapa*, labda ingekuwa bora zaidi. Kama mtu hawezi kuona mambo hayo, mbona, hatuwezi kuwalaumu, vema, hilo ni sawa. Kama nisingeweza kuona chochote, bila shaka nisingesema lolote kulihusu, ningeendelea mbele tu. Jambo la kwanza, ninge—ningeketi chini, nilichunguze katika Maandiko nione kama ilikuwa ni Biblia kwanza, kwa sababu hapo ndipo kweli yote inapotoka, Biblia.

6 Sasa, ibada zetu zijazo, kama ikitokea kwamba kuna mtu hapa, tunaenda Carolina Kusini. . .Carolina Kaskazini kutoka hapa, na halafu Carolina Kusini, kisha California, Canada, na Alaska, ndipo turudi, na tunatumaini kwenda ng'ambo tangu hapo na kuendelea, kwa muda kidogo.

7 Sasa, usiku wa leo, nilikuwa na mambo kadhaa hapa niliyotaka kuzungumzia, lakini muda umeenda, sitazungumza kupita saa nane. Nilikuwa tu nikifanya mzaha. Ni—nitasoma Maandiko machache hapa, juu ya muhtasari fulani ama maelezo na Maandiko niliyoandika, na kutoa maoni machache tu, kisha tuta—tutairudisha ibada hii kwa hawa ndugu. Sasa, mtakuwa mkiniombea, nina—nina hakika, ninategemea hilo, kwamba ninyi—kwamba mnaniombea.

8 Sasa, katika Injili ya Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, kifungu cha 35, ninataka kusoma hadi kifungu cha 41:

> Tena *siku ya pili yake Yohana alikuwa amesimama pamoja na wawili katika wanafunzi wake;*
>
> *Naye* alimtazama *Yesu akitembea,* akasema, *Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu!*
>
> *Wale wanafunzi wawili wakamsikia akinena, wakamfuata Yesu.*
>
> *Yesu aligeuka, akawaona wakimfuata, akawaambia, Mnatafuta nini?* Nao *wakamwambia, Rabi, (maana yake, Mwalimu), unakaa wapi?*
>
> *Akawaambia, Njoni, nanyi mtaona.* Basi *wakaenda,* wakaona *akaapo, wakakaa kwake siku ile, kwa maana ilikuwa yapata saa kumi.*
>
> Basi *Andrea, nduguye Simoni Petro, alikuwa mmoja wa wale wawili waliomsikia Yohana, na wakamfuata Yesu.*
>
> Ndipo *huyo akamwona kwanza Simoni, ndugu yake mwenyewe, akamwambia, Tumemwona Masihi, ambayo, maana yake, Kristo.*

9 Sasa, ninataka kuwashukuru ninyi nyote kwa ajili ya zawadi hii hapa, ambayo bado sijaifungua. Na—na—na halafu hivi majuzi usiku Ndugu Carlson alienda kinyume kidogo na mawazo yangu alipochukua sadaka na kunikabidhi, nami nikapata mahali pazuri, usiku wa leo, kwa ajili yake. Kwa hiyo asanteni sana, hakika ninathamini hilo. Nami najua ya kwamba ikiisha kutoka kwenye yenu, mikono, hadi kwa yangu, inanibidi kuwa msimamizi wa masilahi haya ya Mungu, wa pesa hizi, nami nitaiweka mahali pazuri sana nipajuapo: ambapo jambo fulani linafanywa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu.

10 Baba wa Mbinguni, kumekuwa na mambo mengi sana makuu yaliyosemwa usiku wa leo, Sijui kama una Ujumbe mwingine kwa ajili ya hawa watu, una jambo fulani ambalo lingewatia moyo, ama kuwapa imani. Tumesikia kutoka kwa mashujaa mashuhuri wa hudumani, jinsi nilivyojaliwa kuwa mbele yao usiku wa leo, wanaume wanaokupenda, na wanawake.

11 Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya nyimbo hizo, na kwa ajili ya mioyo, na usikivu wa watu hapa kwenye saa hii iliyochelewa, na wangali wanangojea, wanaona njaa na kiu, Bwana. Kukusikia Wewe ukinena katika lugha ambayo sikujua chochote kuihusu, kumsikia askari hodari akisimama hapa, na kuifasiri; inanitia moyo, Baba, ninashukuru sana kwa mambo haya yote.

12 Sasa, wabariki watu hawa, Baba, na ubariki Neno Lako, na umsaidie mtumishi Wako sasa. Kama kuna mambo machache yanayoweza kusemwa ambayo yangemsaidia mtu fulani, ninaomba ya kwamba Wewe utayatumia sasa, katika Jina la Yesu. Amina.

13 Ninataka kusema ya kwamba wito ulio mkuu sana uliopo duniani, kwa maoni yangu, ni huduma za kimishenari. Mtu yeyote ambaye ni mmishenari ni mtume, kwa maana neno *mtume* linamaanisha "mtu aliyetumwa," na neno *mmishenari* ni "mtu aliyetumwa," kwa hiyo yote mawili ni neno lile lile, ama yanatumika sawa. Na ni kwa nini walipendelea kujiita "wamishenari" sijui, bali ni neno zuri, ama mitume.

14 Sasa, ninataka kuchukua somo, usiku wa leo, kutoka kwa *Kushawishika Na Kisha Kuhusika,* hayo maneno mawili, kutoa maoni machache tu, na kunukuu Maandiko machache hapa juu yake, kwanza kushawishika, na kisha kuhusika. Sasa, kutokana na somo letu la Maandiko tuna mandhari mazuri sana. Hivi niko karibu sana na maikrofoni? Inatoa mshindo masikioni mwenu?

15 Tunaona siku hizi, ya kwamba kuna uasi mkubwa, inaonekana kwamba watu hawana shauku kama walivyokuwa. Wanaanguka kutoka kwenye u—ukweli wa kimsingi wa Biblia, wananinii, inaonekana wanachukuliwa na mkondo. Nami nafikiri wahudumu wote wanaolipenda Neno la Mungu, na kujua ya kwamba Hicho ndicho Kigezo pekee ambacho tunaweza kuwa na hakika kwamba tuko sahihi, si juu ya, nadharia fulani, bali juu ya Neno la Mungu.

16 Huo ndio msingi pekee, kwa kuwa, sitaki kusema jambo hili kukufuru, lakini huko Kusini ilisemwa ya kwamba ndugu mmoja mweusi wakati mmoja alibeba Biblia mkononi mwake ambaye hangeweza kusoma, naye bosi wake akamwuliza, kasema, "Kwa nini unaibeba?"

17 Akasema, "Kwa sababu ninaiamini." Naye akasema, "Ninaiamini kutoka *chalada* hadi *chalada*, na *chalada* pia, kwa kuwa ina 'Biblia Takatifu.'" Naye akasema, "Ninataka kusema jambo lingine, afadhali niwe nimesimama juu ya Biblia hiyo kuliko kusimama Mbinguni."

Mtu huyo akasema, "Ungewaziaje hilo?"

18 Akasema, "Kwa sababu, 'Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.'" Na—nafikiri alikuwa na kitu fulani pale. "Mbingu na nchi pia zitapita," kwa hiyo ni . . . kama

umesimama Mbinguni, huenda ikapita, na dunia, itapita, na, bali Neno halitapita kamwe, kwa hiyo hapo ni mahali pazuri pa kusimama.

19 Hapa Chicago, usiku mmoja, nilimsikia Ndugu Tommy Osborn, ndugu yetu hodari, akisema, "Kama ni. . .ninaamini Neno hili," akasema, "kama isingekuwa ni kukufuru, ningeliweka chini na kusimama juu Yake, kuonyesha ya kwamba nilikuwa nimesimama pale." Nilifikiri hilo lilikuwa hasa, la kupendeza sana.

20 Leo hii tunaona, hata hivyo, ya kwamba watu wanaondoka, wanaliacha Neno, wanaondoka kwenye shauku, inaonekana hakuna shauku kubwa sana Kwake. Tunaona kwamba katika, hata miongoni mwa watu wetu wenyewe, watu, watu wa Full Gospel, kwamba tunafikia mahali ambapo tume—tumeshiba kupita kiasi. Sasa, mtu akilishwa kupita kiasi huwa anasinzia, ni mvivu, rafiki yetu daktari hapo hakika angeweza kukwambia hilo, kama umekula kupita kiasi. Nami nafikiri sisi Wapentekoste tumekula kupita kiasi, tumeona mambo mengi sana makuu, hata yamekuwa ya kawaida kwetu, mnaona.

21 Na kama ilivyosemwa wakati mmoja huko Uingereza, kulikuwa na mshairi aliyekuwa ameandika mashairi ya, jinsi ile. . .jinsi bahari ilivyopendeza, ninii yake. . .na shakwe wa baharini, na jinsi ilivyoakisi uzuri wa anga ndani yake yenyewe. Na—na kwa hiyo, alikuwa akienda, kamwe hakuwa ameiona bahari, lakini siku moja alikuwa akienda zake ufukoni mwa bahari, basi alipokuwa akishuka kwenda zake akakutana na mzee, yule ambaye tungemwita, mzee chumvi, baharia mzee.

Naye akasema, "Unaenda wapi, mtu wangu mwema?"

22 Akasema, "Loo, mimi ni mshairi, nimeandika kuhusu bahari." Kisha kasema, "Sijawahi kuiona bado, nimeandika tu juu ya yale niliyosoma." Halafu kasema, "Ninashuka sasa nipate ujuzi wangu wa kwanza. Ninataka kuyanusia hayo maji ya chumvi, pia na—nataka kusikia mlio wa shakwe wa baharini wakati—wakati anapozunguka a—a—angani, na kuona mawimbi yake yakicheza huku yakirusha mawimbi yake meupe, huku anga za samawati zikijiakisi ndani ya hayo maji."

23 Maskini huyo baharia akasimama pale, na kupuliza kiko chake mara chache, kisha akatema mate, kasema, "Sioni kitu kinachosisimua sana hapo," kasema, "nimekuwa juu yake kwa miaka hamsini, nilizaliwa juu yake," kasema, "Sioni chochote juu yake." Mnaona, alikuwa ameiona sana, hata ikawa ni ya kawaida kwake.

24 Nami ninaamini ya kwamba, usiku wa leo, ya kwamba hiyo ndiyo shida kubwa ya makanisa yetu katika tabaka letu la Full Gospel, hapa Marekani, kwamba tumeona wema mwingi sana wa Mungu hata umekuwa wa kawaida kwetu. Hatuuheshimu

itupasavyo, tunafikiri tunauheshimu, lakini kweli ni—ninaamini ya kwamba "Inatupasa kuyaangalia zaidi hayo tuliyoyasikia, tusije tukayaacha yatuponyoke wakati wowote." Sasa, na—naamini ya kwamba hiyo ni kweli.

25 Na wakati, labda kwa mfano, tendo moja la Mungu hapa, labda mngetoka nje na kusema, "Vema, hilo lilikuwa sawa." Lakini tendo hilo moja, labda, katika msitu fulani huko nyuma katika Afrika Kusini, ama Tanganyika, popote pale, Kenya, lingesababisha labda maelfu kuanguka kifudifudi, na kumpa Mungu utukufu, jambo hilo moja tu likitukia. Kwa hiyo mnaweza kuona mahali ambapo nguvu kuu za, mvuto wa Roho utaenda mahali Neno linapodhihirishwa.

26 Sasa, tumewatuma wamishenari katika nchi za kigeni kwa miaka mingi, niliona jambo lile lile tulipokuja Afrika Kusini, ambako nilifanya umishenari hapa pamoja na ndugu yetu, nasi tuliona nini? Mara nyingi ilikuwa ni kusoma, kuandika, na hesabu. Sasa, nina heshima kuu kwa—kwa Afrika na kwa Waafrikana, pia, ndugu, lakini kile kinachohitajika, kumfanya mtu ambaye hata hajui mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, utamwambiaje lolote, ama kumwongoza kwa Kristo, kuhusu kitini ambacho huenda ukampa, asichoweza kukisoma? Unaona? Anachotaka, yeye husoma juu ya Mungu, ama, naye anajua kuhusu mungu mwingine, na miungu wa kila namna, bali anachotaka ni kitu fulani katika matendo, kitu fulani anachoweza kuona.

27 Hiyo ndiyo sababu mitume walivikwa uwezo, kwa sababu walikuwa katika siku za kipagani, na miungu mbalimbali walikuwa wakiabudiwa, nao walitaka kuona dhihirisho la Mungu wa kweli na aliye hai, ambaye angeweza kujitambulisha Mwenyewe.

28 Kwa hiyo, ninahisi kwamba labda kazi kidogo inapungua kwangu hapa, huku Bwana akinituma hudumani kule, kwa sababu huko Durban, Afrika Kusini, kwenye wito mmoja wa madhabahuni, nilipomwona mvulana jukwaani aliyeponywa . . . Ndipo daktari, daktari wa tiba, akakimbia jukwaani na kusema, "Ninataka kuninii . . . Ulimfanyia nini mvulana huyo?"

Nikasema, "Sikumgusa kamwe."

Naye akasema, "Ninaweza kuelewa saikolojia yako, ama, telepathia, kusoma mawazo yao."

Nikasema, "Daktari, siyasomi mawazo yao," nikiwaambia hayo mambo, na kadhalika, kwa kuwa unajua kinachotukia.

Akasema, "Vema," kasema, "nilimweka mvulana huyo jukwaani, papo *hapo*, yapata dakika tano zilizopita, naye alikuwa na makengeza ya kutisha."

29 Ndipo akaja moja kwa moja kupitia *hapa*, nami nikakutana naye, nami nikasema, "Sasa, maskini huyu jamaa, mtu yeyote

anaweza kuona ana makengeza. Sijui lolote jinsi ya kulifanya, kama ningalikuwa daktari, na ningeweza kufanya upasuaji, bila shaka ningemfanyia huyo mvulana mdogo, lakini," nikasema, "Mimi si daktari." Nami ni—nikasema, "Sasa, kwa, labda kwa karama ya Kiungu ambayo huenda ikamfanya aamini, huenda ikamfanya kuwa na imani ya kutosha kwa ajili ya uponyaji wake."

30 Na nikiangalia, baada ya mambo machache kutukia, na—na ufunuo namna iyo hiyo wa Kiungu, ama kuona maono . . . Wala hakuna mtu angaliweza kukanusha hilo, huduma ya Bwana Yesu ilikuwa imejengwa na hayo. Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Na, "Neno la Mungu," kulingana na Waebrania 4:12, "ni kali kuliko, upanga ukatao kuwili, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo." "Na—nalo Neno linafanyika mwili tunapolipokea," na kadhalika.

31 Kwa hiyo, maskini mvulana huyu, Hiyo ilisema, "Ninaona umetoka kwenye nyumba ya Kikristo, na nyumbani ambako unaingia kwenye maskini . . . " Wanaviitaje vibanda hivyo vidogo wanamoishi? Ninasahau sasa. [Ndugu mmoja anajibu, "Banga."—Mh.] Ati nini? ["Banga."] Banga. Kasema, "Kulikuwa—kulikuwa na picha ya Kristo imetundikwa upande wa kulia wa ukuta."

32 Basi maskini mvulana huyo amesimama pale, naye alikuwa ndio kwanza ale chakula chake, na maskini tumbo lake lilikuwa chafu sana, na, ambapo angeacha chakula chake kiangukie maskini tumbo lake, na—naye alikuwa akiangalia kote, macho yake madogo yamekaa pamoja. Nami nikasema, "Huyu mtoto mchanga, yeye ni Mzulu," kisha nikasema, "lakini baba na mama yake ni wadogo." Ndipo baba na mama wakasimama, na hiyo ilikuwa ni kweli.

33 Kisha kasema, "Sasa, lakini jambo ni kwamba maskini huyu mtoto mchanga, wakati alipozaliwa, alizaliwa akiwa na makengeza." Ndipo mama na baba wakasimama tena huko nje, kwamba hiyo ilikuwa ni kweli.

34 Nikasema, "Mama, wakati huyu mtoto mchanga alipozaliwa, wakati baba alipokuwa akiyaangalia macho yake, na kuyaona, na kumrudishia mama." Ni kweli, waliinua mkono wao.

35 Nikaangalia nyuma, naye mvulana huyo mdogo alikuwa akiniangalia kikamilifu tu alivyoweza kuangalia, nikasema, "Vema, haitanilazimu kumwombea huyu mvulana mdogo kwa sababu tayari ameponywa. Unaweza kupita."

Ndipo maskini daktari mmoja Mwingereza huko nyuma, bila shaka alikuwa na shauku ya kujua hilo. Akakimbia kule upesi sana, naye akasema . . .

36 Naye Bw. Bosworth akasema, "Usifanye hivyo," kasema, "hatuwezi kufanya hivyo sasa." Kasema, "Hatutaki shida yoyote,

maana wametenganishwa, makabila huko nje sasa." Na mamia mengi na mamia na mamia, na maelfu yao walikuwa wameketi kuuzunguka uwanja huo wa mbio za farasi wa Durban, na wengi wakingojea kuombewa.

Ndipo basi, aliposema hivyo, daktari huyu alisema, "Vema, hapa, ninataka . . . " Kasema, "Bw. Branham, ulimfanyia nini mvulana huyo?"

Nikasema, "Hakuna kitu, kamwe sikumgusa."

Akasema, "Vema, alikuwa amesimama *pale*, alikuwa na makengeza, amesimama *hapa*, yeye hana makengeza." Akasema, "Je, ulimhiponozi mvulana huyo?"

37 Nikasema, "Daktari, kama hiponozi itayanyosha macho yenye makengeza, hivi huoni ni afadhali ninyi jamaa mjizoeze uhiponozi kidogo?" Nikasema, "Unajua vema zaidi ya hivyo."

Na—naye akasema, "Vema, mimi—mimi . . . "

Nikasema, "Hivi huamini kuna Mungu?"

38 Akasema, "Hakika, ninaamini Mungu yupo." Kasema, "Mayungiyungi . . . " Mnajua jinsi mayungiyungi yenu makubwa yalivyo mazuri huko Afrika. Kasema, "Ninaamini ya kwamba kama kuna . . . Mungu yuko katika yungiyungi hilo, la sivyo lisingeweza kuishi, lakini," kasema, "ni halisi vya kutosha kumfanya mvulana mwenye makengeza . . . ?"

39 Nikasema, "Vema, itakubidi tu kuamini neno langu kwa ajili yake, hilo tu ndilo ninaloweza kukwambia." Nikasema, "Yule pale amesimama pale, wala sikumgusa kamwe, naye Bwana Mungu, Yeye aliyepo sasa, alimfanya mzima kabisa, naye huyo hapo amesimama, hakuna kitu kingaliweza kusemwa juu yake." Nikasema, "Mwite anayefuata."

40 "Hebu," akasema, "hebu kidogo." Akasema, "Bw. Branham, mimi ni mshiriki tu wa kanisa, kama kuna Mungu aliye halisi vya kutosha ku- . . . kufanya macho ya mvulana huyo yanyoke moja kwa moja jukwaani, ninamtaka awe Mwokozi wangu."

41 Halafu nilipokuwa nikiondoka Durban, yapata majuma matatu baadaye, kulikuwako na maelfu huko nje wakinipungia mkono wa kwaheri, akaruka juu ya ua, akakimbia huko nje, na kunikumbatia kwa mikono yake, na kuanza kunena kwa lugha zisizojulikana. Akasema, "Bwana ameniita kwenye huduma ya kimishenari, kuwa mmishenari wa tiba sasa."

Nikasema, "Bwana asifiwe."

42 Mnaona, hilo ndilo linalohitajika. Hilo ndilo linalotukabili siku hizi. Kusoma na kuandika ni sawa, bali kile watu wanachohitaji ni nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo. Siku hizi tumekuwa tukianguka kupita kiasi, katika nchi hii . . . kwa ajili ya hilo . . . kutoka kwa hilo. Kanisa limeanguka kutoka kwake, sasa, halilijali, watu hawaonekani kulitaka.

43 Wanaona mambo mengi ya bandia yanayoendelea, hakika. Ni wangapi waliowahi kusoma *Maisha Ya Martin Luther?* Nilikuwa nikisoma maishani mwake, nacho kilisema halikuwa jambo geni, sana, ya kwamba Martin Luther angeweza kulipinga kanisa Katoliki na kupita nalo, lakini jambo la kushangaza, kwamba angeweza kushikilia kichwa chake juu ya ulokole wote uliofuata uamsho wake, na bado adumu safi, na dhahiri pamoja na Neno. Jambo ndilo hilo, mnaona, dumu tu na Neno, Hicho ndicho Kitu kinachokuongoza utoke nje, maana Mungu ni Neno, unaona. Na—nasi tunajua ya kwamba Kristo ni Neno.

44 Lakini leo hii, kwa namna fulani ni, badala ya sana sana kuwapeleka watu kwenye Neno, na kwa Mungu, na kwa Biblia, ni, "Njoo ujiunge na kanisa." "Unga mkono kipindi *fulani* cha redio." Ama—ama, "Jenga majengo makubwa." Mnajua jinsi ilivyo.

45 Nanyi mnajua kile ninachoamini ndicho sababu ya jambo hili? Ni kwa sababu bado hawajashawishika ya kwamba ni Mungu pamoja nasi, ninaamini hilo. Ninaamini ya kwamba watu kweli hufanya hivyo kwa uaminifu, na wanafikiri ya kwamba Mungu yuko katika harakati za kuunda makanisa, na kuunda madhehebu makubwa, na—na kuingiza watu wengi zaidi, na kujenga majengo mazuri zaidi, na kadhalika namna hiyo, ya kwamba huo ni mpango wa Mungu.

46 Huo si mpango wa Mungu, kamwe haukuwa. Kamwe hakutuagiza kufanya hivyo, ingawa ni mizuri hivyo. Kamwe hakusema, "Enendeni ulimwenguni kote mkajenge shule," hata hivyo, tunazipenda, zote ni sawa, zinaninii . . . Kamwe hakusema, "Enendeni mkajenge hospitali," hata hivyo, Mungu ashukuriwe kwa ajili ya kila moja yazo. Hiyo ni kazi ya watu wengine, lakini ya mhudumu ni: "Ihubiri Injili. Nayo Injili inakuja si katika Neno tu, bali kwa nguvu, na dhihirisho la Roho Mtakatifu." Hilo ndilo agizo: hilo kwa *umishenari*, na daima, *umishenari* ni sahihi. Naam.

47 Loo, watu wanaamini, bila shaka, kwamba wanaamini mambo hayo, lakini wao, kama vile maskini mama yangu wa kusini alivyozoea kuniambia, "Matendo yako hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno yako." Hiyo ni kweli. Tunapoona kwamba watu wanaikataa Injili, unawezaje kusema unaamini Injili, unapokataa jambo lile lile unalosema unaamini? Kamwe haifanyi kazi.

48 Sasa, Yesu alisema, "Kama unanipenda, walishe kondoo Wangu." Mnaona? Sasa, hatutaki kuwalisha miradi ya elimu, wala sitaki kuwalisha magugu ya kimadhehebu. Lakini, kondoo hula Chakula cha kondoo, hicho ndicho kinachohitajika kumfanya kondoo anenepe, ni Chakula cha kondoo. Hiyo ni hakika. Vema. Nacho Chakula cha kondoo ni Injili, mahubiri ya nguvu za kufufuka kwa Bwana wetu Yesu Kristo, kumleta Yeye

Mwenyewe kwa watu. Yeye hajafa, Yeye yu hai, na yu hai milele. Yuko hapa usiku wa leo, na hiyo ndiyo Injili.

49 Kwa nini Yohana alikuwa na hakika sana, kwa saba-... kwamba alijua ya kwamba Huyu alikuwa ndiye Masihi? Kwa sababu kwanza, *alishawishika* ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi. Huwezi—huwezi kufanya mengi sana mpaka umeshawishika, ndipo unahusika. Lakini mpaka utakaposhawishika, huhusiki sana.

50 Nina hakika, usiku wa leo, kwamba watu ambao wangekosoa uponyaji wa Kiungu, ambao wangekosoa kupaza sauti, ama kitu kingine chochote ilicho nacho Biblia, ama karama za Roho, sababu ya wao kukikosoa, ni kwa sababu, ama kutohusika nacho, ni kwa sababu hawajashawishika bado kwamba ni kweli. Lakini acha litendeke kwako wakati mmoja, ndipo basi utajua shida ya watu hawa, utaona basi, kama itawahi...Mtu fulani alisema hawaamini katika uponyaji wa Kiungu, bado hujawa mgonjwa vya kutosha, hivyo tu, wewe... hilo ni jambo moja la hakika.

51 Ninawaona watu wengi sana wanaosema kwamba ugonjwa ni baraka. Mwulize daktari fulani kama ndivyo. Ni kwa nini basi, unaenda, kama una ugonjwa wa kidole tumbo, halafu hiyo baraka inakatiliwa mbali? Hakika nisingetaka kufanya hivyo, hilo kidogo ni kinyume cha nadharia yako mwenyewe. Ati baraka ikatiliwe mbali? Nisingetaka kufanya hivyo, ningeiweka tu na nife, mnaona. Lakini ugonjwa si baraka, ugonjwa ni laana ya ibilisi, naye Yesu alisema ulikuwa ni laana. Vema.

52 Sababu ya Yohana kuhusika sana, ni kwa sababu alishawishika ya kwamba wakati wa kukaribia kwa Masihi ulikuwa umewadia, kwa sababu huko nyikani alikuwa ameambiwa ya kwamba angemtambulisha huyu Masihi. Naye alishawishika kabisa kwamba alikuwa sahihi, na alikuwa kwenye wakati mzuri kabisa. Ninapenda hilo. Mnaona?

53 Kama umeshawishika, unajua ya kwamba umeshawishika kabisa, basi unahusika juu ya yale unayozungumzia. Mtu anawezaje kuihubiri Injili ambaye kweli hajashawishika kwamba kabisa anayo Kweli? Ungewezaje kufanya hivyo? Lakini unaposhawishika kwamba unajua! Nawe unawezaje kushawishika, kama si kulingana na Maandiko? Huna budi kushawishika, ndipo basi unahusika; hilo ndilo linalokufanya uhusike ni kwa sababu umeshawishika.

54 Alijua wakati wake ulikuwa umewadia, naye alijua ya kwamba Ujumbe wake ulikuwa wa kuhubiri toba. Na kwa hiyo, alishawishika, na kwa hiyo akahusika kuutangaza Ujumbe wake kabla ya kule kuonekana kwa Masihi. Sasa, yeye hakuhusika, Yohana hakuhusika, katika majengo makubwa, ama miradi ya elimu, ambayo ni sawa, walikuwa nayo, walikuwa na watu walioishughulikia hiyo, walikuwa na kuhani, na marabi, na

wajenzi, na wasomi wa siku hizo, wangeweza kushughulikia hiyo, lakini kwa Yohana, alishawishika ya kwamba Masihi alikuwa mahali fulani wakati huo, papo hapo duniani. Naye alishawishika ya kwamba hawana budi kutubu na kuinyosha njia kwa ajili ya Kuja Kwake, kwa hiyo alihusika na kuutangaza Ujumbe.

55 Hiyo inapaswa kuwa ninii. . . Kama tunaamini ya kwamba kuja kwa Masihi kumekaribia, nafikiri tunapaswa kuweka kando kila kitu kingine, na tujishughulishe na kuupeleka Ujumbe huu kwenye nchi za ng'ambo upesi tuwezavyo, hiyo ni kweli, kama tumeshawishika. Lakini tunahubiri ya kwamba Masihi anakuja na tunataka kuweka dola milioni mia moja katika jengo. Na kama Masihi yuaja, hiyo itafaa nini, kama tunaamini?

56 Mnaona, ninii hasa, ushuhuda wetu, matendo yetu hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno yetu. Kama nilikuwa na dola milioni mia moja, nami niliamini Masihi yuaja, ningeunga mkono mpango wa kimishenari ambao ungeenea kote nchini upesi sana, na kuliweka Kanisa tayari kwa ajili Yake, ningefanya hivyo, kwa hiyo nimeshawishika ya kwamba Masihi yuaja upesi, nami ninahusika kuhusu Injili kufika kila mahali ninapoweza kujua inaweza kufikishwa.

57 Ninavutiwa na mipango ya kimishenari, hiyo ndiyo sababu niko hapa usiku wa leo, kuweka maneno yangu ya Injili pamoja na Ndugu Joseph, na hawa wamishenari wengine, ni kuona ya kwamba Neno hili linatoka, maana halina budi kwenda kwa kila jamaa, kabila, na taifa kabla Yeye hajaja, Naye anangojea hilo sasa. Siamini mpango Wake ni kujenga majengo, ama mambo ya elimu kanisani, ninaamini ni kuipeleka Injili kule, kwa kuwa Yeye anaingojea. Wakati umepita, naamini huu ndio wakati wa kufanya jambo hilo.

58 Yohana alijua ulikuwa ni wakati wa kuwa. . . kutubu, kuomba toba, na kujiweka tayari kwa ajili ya Masihi. Na kama ulikuwa ni wakati wa toba wakati huo, na sasa je? Kuja kwake kulikuwa kumekaribia, Yeye alikuwa pamoja nao wakati huo. Sasa, angalieni ni karibu jinsi gani. . . Hebu tulinganishe hili kwa muda kidogo tu sasa.

59 Yohana alikuwa na hakika sana ya kwamba kuonekana kwa Masihi kulikuwa kumekaribia sana, ama, kuja Kwake kulikuwa kumekaribia sana, hata akasema, "Kuna Mtu aliyesimama miongoni mwenu sasa, yupo Mtu miongoni mwenu sasa msiyemjua, na Yeye Ndiye Yule atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto." Sasa, Yohana hakuwa anamjua bado, bali alijua kuja Kwake kulikuwa kumekaribia sana hata tayari alikuwa katikati ya watu.

60 Hebu niseme hivyo, enyi marafiki. Na ndugu zangu, mbona mnanihukumu? Wakati Yesu, Mwenyewe (Nimewaambia mara

ngapi?), aliahidi, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Hivi Yeye hakuahidi kitu kiki hiki mnachoniitia "mchawi," ama kitu fulani kukihusu? Hivi Yeye hakuahidi hilo lingetukia? Basi nini?

61 Tunaona huko Sodoma wakati Malaika watatu waliposhuka kwenda kuuhubiri Ujumbe (Na kulikuwako na matabaka matatu ya watu, daima, hao ni, waaminio, wasioamini, na wanaojifanya waaminio, hiyo ni . . . wao daima wako pamoja, nao wanashirikiana pamoja, kwa namna fulani wa—wametupwa pamoja.), sasa, kulikuwako na hao Watu wawili kati yao walioshuka na kuhubiri Sodoma, kwa Lutu. Huyo alikuwa ni yule mwanamwali wa kawaida aliyelala, uwakilishi wake. Nao wakahubiri toba, na kamwe hawakufanya mwujiza sana, waliwapofusha watu, bila shaka, kuhubiri Injili humpofusha asiyeamini, tunatambua hilo.

62 Na Billy Graham mamboleo, kama huyo, aliingia katika mji huu hapa, na yeye, Mungu amembariki, na kumtuma kama mjumbe kwa ulimwengu wa kimadhehebu. Naye hachezi, analiweka moja kwa moja mle ndani, hivi kwamba, ameshika sana Neno la—la toba si kama mtu yeyote nimjuaye, angalau, kumsikia akihubiri. Vema, mbona? Hiyo ndiyo huduma yake, hivyo ndivyo anavyopaswa kufanya. Lakini hiyo bila shaka iliwakilisha kile Watu hao walichokuwa nacho kule chini, katika kuthibitisha huduma yao; lakini Mmoja alibaki nyuma.

63 Sasa, Ibrahimu anawakilisha Kanisa ambalo haliko Sodoma, bali liko nje ya Sodoma. Neno *Kanisa* linamaanisha "walioitwa watoke." Na kuna kundi la watu ambao wameitwa kutoka katika maisha ya namna hiyo, kutoka katika mambo hayo, kutoka kwenye madhehebu hayo, hawa hapa: Waepiskopalia, Wapresbiteri, Wakatoliki, mimi Mbaptisti, nilikuwa, na mambo haya yote, mnaona, *walioitwa watoke*, "wateule, waliowekwa kando," nao wako mbali na kitu hicho.

64 Sasa, angalieni yule Mjumbe, aliyewajia, Yeye alisema, "Ibrahimu," si Abramu, siku chache kabla ya hapo Mungu alikutana naye na kubadilisha jina lake kutoka Abramu likawa Ibrahimu, Sarai likawa Sara, naye akasema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?"

Ndipo Ibrahimu akasema, "Yuko hemani," nalo hilo hema lilikuwa nyuma Yake.

65 Naye akasema, "Nitakuzuru kulingana na muhula wa uhai." Kwa maneno mengine, "Utampata mtoto huyu mchanga ambaye umemngojea kwa miaka ishirini na mitano."

66 Naye Sara ndani ya hema, akacheka moyoni mwake, na kusema, "Mimi, mwanamke mkongwe, ninaweza kupata raha na bwana wangu, naye ni mzee?" Alikuwa na miaka tisini, naye mume alikuwa na mia moja. Mwulize tu mtu yeyote, hilo

limepita hoja zote kwa mbali sana, alikuwa amekoma hedhi kwa muda wa miaka ishirini au thelathini, na mwili wake ulikuwa kama uliokufa, hata hivyo, "Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini," bali aliamini Neno la Mungu, haidhuru.

67 Sasa, hilo linapaswa kuwakilisha Kanisa siku hizi. Kupitia mwana huyo aliyeahidiwa Yeye alimzaa Mzao wa Kifalme, ambaye alikuwa ni Kristo. Na kupitia hapo akamwingiza nanii. . . akamfanya baba wa mataifa, ambao ni Kanisa la Mataifa, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Nasi tunadai kuwa Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, na kuona Neno Lake likithibitishwa mbele zetu, kisha tunakataa kulisaidia, ama—ama kuliunga mkono, au—au hata—hata tunalikana? Tunawezaje kuwa Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu na kufanya ujanja kama huo?

68 Angalieni kile kilichotukia. Naye akasema . . . Sara akacheka na kusema, "Mimi, mwanamke mkongwe, na nipate raha na bwana wangu, tena?"

Naye Malaika, huku amemwelekezea mgongo Wake, akasema, "Kwa nini Sara akacheka?"

69 Sasa, Yesu alisema . . . Sasa, tunataka kwanza kujua Mtu huyo alikuwa ni Nani. Hailitaji Jina Lake, bali Ibrahimu, aliyezungumza Naye, akamwita, "Mungu." Neno lililotumiwa, "Elohimu." *Elohimu* katika Ki—Kiebrania, nafikiri, ni "Ajitoshelezaye Kwa Yote," Yule—Yule Mkuu, "Elohimu, yule Mungu Mkuu Mwenyezi." Na kama Ibrahimu, aliyekutana Naye, alimwita hivyo . . .

70 Sasa, hilo liliwakilisha nini? Kwamba ulimwengu wa kawaida, kungekuwa na Sodoma na Gomora. Sasa, kumbukeni, hiyo ilikuwa ni kabla ya ule Moto kushuka. Tumeahidiwa Moto wakati huu. Na kabla halijatukia wale wajumbe wakashuka, na kulihubiria kanisa ambalo lilikuwa lingali katika hali ya kawaida huko Sodoma. Nayo Biblia ilisema ya kwamba dhambi za mji huo hata ziliitesa nafsi, nafsi yenye haki, ya Lutu kila siku.

71 Lakini Yule aliyekuja kwa Kanisa teule alifanya ishara ya namna hiyo, naye Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Na hata hivyo, hawalioni. Siwezi kulielewa. Vema.

72 Kumbukeni, ya kwamba leo hii, kwa sababu kwamba mnaona Kanisa likipanda kutoka jambo moja kubwa hadi lingine kubwa . . . Na watu hao wakati mwingine hujenga ua kidogo. Kama Luther kamwe hakuwa amejenga ua, angekuwa Mpentekoste siku hizi. Kanisa la Kipentekoste, leo, ni kanisa la Kilutheri lililoendelea mbele. Hiyo ni kweli kabisa.

73 Sasa, tunajenga nyua. Kama tungeunda madhehebu yetu, na kumalizia fundisho letu kwa koma, "Tunaamini *hili*, pamoja na kadiri Mungu atakayotupa," hilo lingekuwa sawa, bali wanalimalizia kwa kituo, "Tunaamini *hili*. Basi wewe uliamini,

la sivyo usije karibu nasi." Kwa hiyo basi, Mungu, unajifungia tu nje. Sawa.

74 Lazima tuwe tayari na wazi kumpokea Mungu, na chochote Mungu alicho nacho kwa ajili yetu, kwa moyo mkunjufu, hatuna budi kukipokea. Na kwa hiyo wakati mataifa hapa yanalikataa Neno la Mungu, kuna makafiri huko ng'ambo walio tayari kulipokea. Nayo Injili itatoka kwenye taifa hili la kielimu iwaendee makafiri wasiojua mkono wa kulia wala wa kushoto, na hilo ndilo linalotendeka sasa hivi, kweli kabisa, linaondoka.

75 Sasa, Yohana alikuwa na hakika *sana* ya kwamba atamwona Masihi, hata akasema, "Yuko miongoni mwetu sasa." Sasa, tazameni, angalieni, kuna tofauti kubwa sana katika ishara ya kuonekana kwa Yesu, halafu kuja kwa Yesu. Hayo hapo maneno mawili tofauti, yanamaanisha mambo mawili tofauti, *kuonekana* kwa Bwana, na *kuja* kwa Bwana.

76 Sasa, kuonekana kwa Bwana ni sasa, wakati Yeye anapoonekana katika watu Wake, Roho Wake akitenda kazi miongoni mwao, akithibitisha ya kwamba ni Yeye aliye pamoja nao, akiwatayarisha kwa ajili ya Unyakuo, kwa ajili ya kuja kwa Bwana kumnyakua Bibi-arusi, mnaona, *kuonekana* na *kuja*. Vema.

77 Sasa, sasa, jambo hili linatupasa kufanya, kama tunaweza kuliamini, na kulijali, kwanza hatuna budi kushawishika ya kwamba ni Mungu, ndipo tunaposhawishika, basi tunahusika. Ninapenda hilo.

78 Vema. Yohana alijua kile Yeye angekuwa, alimtazamia, kwa sababu Mungu alimwambia huko nyikani, "Kutakuwa na ishara itakayomfuata." Na wakati Yohana alipoiona ishara hiyo, alijua ya kwamba Masihi alikuwa amesimama pale mahali fulani, naye akaiangalia, mahali ilipoelekea, naye akasema, "Huyo hapo Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Kwa kuwa Yeye aliyeniambia nyikani, 'Yule ambaye utamwona Roho akishuka, na kukaa juu Yake, Huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.'"

79 Sasa, Biblia inaahidi katika siku hizi za mwisho ya kwamba mambo haya, mnayoyaona leo, yatakuwa yakitukia. Ndipo tunaona kutokea kwa Masihi katika umbo la Roho Mtakatifu Kanisani. Na kama uhai wa—wa mpea ulikuwa katika mkuyu, ungezaa kitu kile kile, ungezaa peasi, kwa sababu uhai ndani ya huo mti ungekuwa, sasa, ungekuwa uhai wa mpea. Haidhuru ni mkubwa jinsi gani, ni mdogo jinsi gani, uko katika umbo gani, ungekuwa vile vile, maana uhai ulio ndani yake huzaa matunda yake. Nalo tunda la Roho humfuata Roho, ama Roho huzaa tunda na ishara za Injili.

80 Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Zingefuatana nao. Na kwa muda gani? "Ulimwenguni kote, na kwa kila taifa."

81 Andrea, kama tulivyosoma habari zake hapa dakika chache zilizopita katika kuja kwa Bwana, Andrea, yeye alikuwa tu Mwebrania wa kawaida aliyeenda kule kumwona, kumsikiliza Yohana akihubiri, naye alikuwa na hakika ya kwamba nabii huyu alijua alichokuwa akizungumzia. Ndipo basi, jukwaani, siku moja, akaja Yesu, naye akamsikia Yohana akimtangaza, na kusema, "Huyo hapo, Huyo Ndiye papo hapo."

82 Naye Andrea, akasema, "Sasa, jambo ninalopaswa kufanya ni kutomkosoa Yohana, ama—ama kuchukua hilo tu, bali nitaambatana Naye nipate kujua." Laiti kila mtu huku Chicago angekuwa mwaminifu hivyo.

83 Sasa, Andrea alikaa pamoja Naye usiku kucha. Hivi mliona katika Maandiko? "Alikaa pamoja Naye usiku kucha." Alikaa mpaka aliposhawishika. Na baada ya kushawishika, ndipo akahusika kuhusu mtu mwingine kuwa na kitu kile kile alichokuwa nacho.

84 Lakini mtu hana budi kushawishika kwanza, na kitu pekee cha kushawishi ni dhihirisho, ama utambulisho wa Injili ikitambulishwa ndani yako. Unapoona ya kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani na kuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu, huo ndio utambulisho wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli kabisa. Roho Mtakatifu anawezaje kuandika Biblia kisha ageuke, akane yale aliyoandika? Unaona, Yeye hawezi kufanya hivyo. Yeye ni. . .Huo—huo ndio utambulisho wa kutokuamini, huo ndio utambulisho wa kutokuamini. Lakini utambulisho wa imani, Yesu alisema, "Ishara hizi zitawatambulisha hao waniaminio Mimi." Sasa, tunajua ya kwamba hilo ni Neno la Mungu Mwenyewe. Vema.

85 Andrea alihusika kuhusu ndugu yake, baada ya kukaa na Yesu usiku kucha. Ninahofia kwamba, laiti tungalikuwa na wakati zaidi, lakini, ninahofia kwamba hiyo ndiyo shida ya makanisa yetu siku hizi, Ndugu, Dada, kamwe hatukai muda mrefu vya kutosha, tunaingia mbio na kupeana mikono na mchungaji, tunaandika jina letu kwenye kitabu, kisha tunaenda nyumbani; tunajiita mfuasi wa kanisa bila mzigo kwa waliopotea hata kidogo.

86 Hatujali kuhusu umishenari wa ng'ambo, hatuhusiki juu ya walio na njaa mahali pengine popote. Tumejaza matumbo yetu, nasi tuna kanisa zuri, lenye joto, la kupendeza, na mchungaji mzuri, mwenye akili ambaye kamwe asingesema lolote dhidi ya mambo tunayofanya, kwa hiyo sisi, inaonekana tumeridhika sana. Mnaona? Kwa hiyo hatuhusiki, hatuhusiki kwa yale yanayoendelea.

87 Lakini kama ulishawishika ya kwamba Yesu Kristo alifufuka katika wafu, na atakuhukumu kwa ajili ya dhambi zako, na kwamba Kuja Kwake kumekaribia, na huyu ni Roho Mtakatifu akijitambulisha Mwenyewe, basi ungehusika kuhusu

watu wengine pia, na kuwaleta Kwake, kuhusika tu kama—kama vile Andrea alivyohusika.

88 Ilikuwa ni Yakobo, hakuhusika sana kuhusu alivyokuwa amemfanyia ndugu yake, mpaka usiku mmoja alipopigana mwereka usiku kucha. Alikuwa laghai kidogo, kama nilivyomwita mara nyingi, samahani kwa usemi huo, lakini ye—yeye daima alikaa karibu na mama yake, naye Esau alikuwa, alifanya kazi, kisha akaiba haki ya mzaliwa wa kwanza kutoka kwa Esau na kutoroka, na baada ya kitambo kidogo hakuhusika, alikuwa akifanikiwa, akifanya vema, lakini usiku mmoja alikutana na Mungu, wala hakumwachilia, hakusema, "Loo, ninaihisi. Loo, a—afadhali niondoke *hapa*."

89 Tofauti kati ya Yakobo na wengi wa watu siku hizi, Roho Mtakatifu atashuka juu ya mwenye dhambi, na, ama asiyeamini, ama mkosoaji, na kujaribu kumshawishi, na itakuwa kama Mt. Agostino wa Hippo. Badala ya kuendelea mbele wakati alipokuwa kule kwenye kanisa la Ireneo, na kumpokea Roho Mtakatifu, alishuka akaenda Afrika, hadi Hippo, Afrika, tena. Naye ndiye aliyetoa lile tangazo kwamba ilikuwa ni sawa kuwaua Wakristo ambao hawakuamini katika kanisa la Kirumi.

90 Na kwenye historia ya wafia imani, leo hii, wamesimama watu milioni sitini na nane waliouawa na hilo kanisa. Mnaona? Kwa nini? Alikuwa na nafasi ya kumpokea Roho Mtakatifu, alikuwa na nafasi, bali hakushawishika kwamba Huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu, nanyi mnaona mahali kuhusika kwake kulikoelekea.

91 Yudasi alikuwa na nafasi ile ile hao wengine waliyokuwa nayo, bali hakushawishika ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi, kwa hiyo mnaona kilichotukia. Hakuhusika na jambo Hilo, kumhusu Yeye, kwa sababu hakushawishika kabisa kama alikuwa sahihi au la. Sasa, hatuna budi kushawishika.

92 Baada ya Yakobo kupigana mwereka usiku kucha, badala ya kujaribu kumpiga vita Mtu huyo, Yakobo alimshikilia. Loo, laiti tungalikuwa na yapata nusu saa juu ya hilo, jinsi ambavyo mtawala huyo mpigana mwereka, a—alivyoweza kushikilia mpaka akapata alichokuwa akitafuta. Alishikilia *mpaka*! Ilichukua usiku kucha, lakini alikaa pale. Alitaka kushawishika kabisa, na wakati alipokaa mpaka Mungu alipobadilisha mwenendo wake, alishawishika.

93 Hiyo ndiyo shida yetu siku hizi, hatukai muda mrefu vya kutosha mpaka tushawishike kutembea kwetu, hatutembei kama Wakristo. Kama tukikaa pamoja Naye muda mrefu vya kutosha, atakufanya utembee tofauti, uzungumze tofauti, uishi tofauti, utende tofauti, uamini tofauti, uwe tofauti. Jambo ni kwamba hatukai muda mrefu vya kutosha, hatushikilii.

94 Yakobo alishikilia, akasema, "Niachilie, sina budi kwenda."

95 Akasema, “Sitakuacha mpaka nitakaposhawishika kabisa.” Amina. Ndipo unapochukua ahadi ya Mungu na kuishikilia hiyo mpa-. . . usimwachilie, kaa tu hapo mpaka utakapomwona Mungu akijitokeza jukwaani, ndipo umeshawishika. Na wakati unaposhawishika basi unahusika kuhusu wengine, kuna kitu fulani kuhusu hilo kinachokufanya uhusike.

96 Yakobo alituma mifugo, na kila kitu kingine, kukutana na ndugu yake, alihusika kuhusu masilahi ya ndugu yake, baada ya kushawishika kwamba kuna Mungu, baada ya kushindana mwereka na Yeye mwenyewe. Tunahitaji jambo hilo.

97 Shamgari, wengi wenu hamjawahi kusoma, ni kama tu aya moja katika Biblia, sentensi ndogo ndiyo yote yaliyoandikwa kumhusu. Yeye, nafikiri alikuwa yapata mwamuzi wa 13 wa Israeli, Shamgari.

98 Katika siku hizo Wafilisti wangeingia, wakati waamuzi walipowaamua Israeli. Wafilisti wangekuja yapata, wakati Israeli walipokuza mazao yao yote, kila kitu kimewekwa ghalani, kila kitu ni sawa, hao Wafilisti wangekuja moja kwa moja barabarani, wawanyang’anye, nazo familia zao zingepata njaa. Na kuwanyang’anya, mwanamume akisema lolote, wangemwua, waingie moja kwa moja ndani, wawaue wanawake, wawabake wasichana, na kadhalika, wachukue chakula, warudi nchini mwao wenyewe, na kuishi kwa anasa, naam, majira yote ya baridi kali. Kama wangewaacha waishi kule, wangekufa kwa njaa, kwa kweli.

99 Vema, labda mwaka baada ya mwaka hawa Wafilisti waliwajia. Maskini, maskini mzee Shamgari, a—alikuwa amesimama huko nje siku moja, na mara alipoweka ngano yake yote, yote imepurwa, imewekwa ghalani, ndipo akasikia kitu fulani kikija barabarani. Alikuwa tu akimwangalia, labda, mke wake, mikono yake ya nguo imetokeza, na msichana wake mdogo, uso mwembamba, uliodhoofika kutokana na ukosefu wa chakula, alihusika juu yao.

100 Na sasa, muda si muda mwajua, huku wakija barabarani, alisikia vishindo vya miguu, akaangalia nje. Ni nini kilikuwa kinakuja kutukia? Wakaja Wafilisti mia sita wenye silaha, wakija kuchukua akiba yake yote ya msimu wa kiangazi, wachukue chakula chake cha majira ya baridi kali. Alijua mke wake angekufa kwa njaa katika hayo majira ya baridi kali, huenda watoto wake wakafa, wangekufa kwa utapiamlo. Naye alijua jambo fulani lingetukia, alihusika kuhusu familia yake.

101 Sasa, kuna jambo moja analopaswa kufanya, kushughulikia hali hii, alitafakari kwa dakika moja, “Ngoja kidogo, mimi si askari, sijui lolote jinsi ya kutumia upanga wala chochote kile, na kuna mia sita dhidi yangu. Ningefanyaje jambo hilo? Nimesimama hapa nimevaa jozi ya nguo za mkulima,” kama ovaroli, ama kitu fulani, “nao wote ni mashujaa waliofunzwa

vizuri, wamevaa helmeti kubwa mno, na maderaya ya kifua na kadhalika, wamefunzwa kama jeshi moja kubwa."

102 Akasimama pale, alihusika kuhusu familia yake, lakini baada ya kitambo kidogo akashawishika, amina, ya kwamba alikuwa na haki. Alikuwa ni Myahudi, alikuwa ametahiriwa, alikuwa katika agano pamoja na Mungu kupitia ahadi aliyompa Ibrahimu, basi alikuwa na haki kwamba Mungu angemlinda na adui zake. Roho akaja juu yake, akanyakua konzo la ng'ombe, hicho ni kitu kidogo wanachomkutua maksai kwacho, alichukua konzo hilo la maksai na kuruka nje ya mlango, na kuwaua Wafilisti mia sita. Ilikuwa ni kitu gani? Alishawishika. Amina.

103 Kama kundi hili la watu hapa, usiku wa leo, lingeweza kushawishika kiasi hicho kwamba Mungu ambaye angeweza kumfanya mwanamke hapa anene kwa lugha, na mwanamume aseme jambo ambalo lingeweza kutabiri, ama kubashiri, nazo nguvu za Mungu ziingie upesi na kuwachukua wenye dhambi na kufanya Wakristo kutoka kwao, kama tungeshawishika kabisa ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu, kungekuwa na maradhi. . . kungekuwa na uamsho utakaoipiga Chicago. Tukiwa na watu hawa wengi wangetufunga sote gerezani kabla ya mapambazuko, maana ingewasha moto mahali hapa kwa Injili na ushuhuda wa nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo. . .?. . . Ungehusika sana!

104 Hatuna budi kushawishika ya kwamba *Hili* ni Neno la Mungu. Usichukue yale madhehebu fulani yaliyosema juu Yake, chukua yaliyo BWANA ASEMA HIVI. Wangeweza kuwa wamekosea, *Hili* haliwezi kukosea, na kama *hilo* ni kinyume na *Hili*, basi *hilo* ni kosa na *Hili* ni kweli, Biblia hii ninayoelekezea, *Hiyo* Ndiyo kweli.

105 Mungu alitoa ahadi, na wakati Mungu alipompa a—ahadi Ibrahimu, na kuninii. . . Alisema angemiliki lango la adui yake, na kwa hiyo Shamgari aliamini hilo. Basi angalieni yale yaliyomkabili! Mungu anahitaji tu mtu mmoja, acha tu amchukue mtu mmoja mkononi mwake, ulimwengu utafikiri yeye ana kichaa, bali ataiendeleza Injili, wakati ameshawishika kabisa ya kwamba Yesu Kristo anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele. Chini ya kitu kingine chochote atasimama mwaminifu na kuendelea, kwa sababu ameshawishika kabisa ya kwamba Mungu ni Mungu.

106 Kama aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Kama Yeye si Mungu jinsi alivyokuwa, Yeye kamwe hakuwa Mungu. Hiyo ni kweli. Yeye ni Mungu asiye na kikomo, mwenye nguvu zote, Mwenyezi, aliyepo kila mahali, ajuaye yote, asiye na kikomo, loo, jamani, Yeye ni—Yeye ni Mungu! Yeye ni Mungu yeye yule aliyeifungua Bahari ya Shamu, Yeye ni Mungu yeye yule aliyemtoa Danieli katika tundu la simba, Mungu yeye yule aliyewatoa wana wa Kiebrania kutoka kwenye ile tanuru ya

moto, Yeye ni Mungu yule yule aliyemfufua Yesu Kristo kwenye asubuhi ya Pasaka, Yeye ni Mungu yule yule aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste, Yeye ni Mungu yule yule aliyemfufua Lazaro kutoka kaburini, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Nami nimeshawishika ya kwamba *Huyu* ni Roho Mtakatifu.

107 Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, "*Hili* ni *Lile*." Kama *Hili* si *Lile*, nitaliweka tu *Hili* mpaka *Lile* litakapokuja, kwa kuwa ninaamini *Hili* ni *Lile*. Nimeshawishika ya kwamba ni Injili, na nguvu, dhihirisho la ufufuo, la kuonekana kwa Bwana Yesu katika siku hizi za mwisho, akilifanya Kanisa tayari kunyakuliwa katika Bibi-arusi. Loo, jamani!

108 Vipi kama Shamgari angekuwa amesema, "Sasa, ngoja kidogo! Sina budi kungojea mpaka, ninawaona wakija, lakini afadhali niondoke, na, niende shuleni kwa muda kidogo, na kujifunza jinsi ya kufanya pambano la kanuni za imani za kimadhehebu, nipate kupigana nao"? La. Kama angalifanya hivyo, hayo tu ndiyo angalijua, kwa hiyo kamwe asingefanya kazi hiyo kwa kupigana kwake.

109 Yeye aliamini tu ahadi ya Mungu, ya kwamba angemiliki lango la adui yake, naye akasimama pale akiwa na hilo konzo la ng'ombe, kile kilichokuwa mkononi mwake, na kukatakata na kupenya hata kufikia ushindi, amina, maana alishawishika ya kwamba kama Mungu aliwahi kuwa Mungu, Yeye alikuwa angali ni Mungu.

110 Hivi hamjashawishika, usiku wa leo, ya kwamba Mungu aliyekuwa katika Agano la Kale ndiye Mungu wa Agano Jipya, na ni Mungu yeye yule leo? Biblia ilisema katika Waebrania 13:8, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

111 "Musa alihesabu kushutumiwa kwa Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri." Kwa hiyo akakiacha kiti cha enzi, akachagua kujiunga na watumwa maskini, wasio na maarifa wala elimu. Kwa nini? Aliuhesabu Utajiri wa Kristo kuwa ni Hazina kuu, Uzima wa Milele, kuliko kuwa na utukufu wake katika ulimwengu huu, wakati huo.

112 Wana utukufu wote wanaotaka, bali kile Mungu anachotaka leo hii ni wanaume na wanawake ambao hawavutiwi na mapambo makubwa mno, na mambo haya mengine yote, na kujenga milioni moja zaidi kwa ajili ya shirika fulani, bali mtu ambaye atachukua Neno rahisi la Mungu na kulihubiri kwa yote yaliyo ndani yao, na kumngojea Mungu kwa ajili ya nguvu za Mungu kujidhihirisha Mwenyewe, na kujionyesha Mwenyewe Mungu yeye yule aliyewahi kuwa. Amina.

113 Shamgari angalingoja mpaka amejifunza kanuni zote za imani na kadhalika, hayo tu ndiyo angaliweza kukabiliana na Wafilisti kwayo, bali kamwe hakungojea. La, bwana.

114 Loo, tunawatuma wamishenari wetu leo. Angalieni tofauti katika kujaribu kuwatuma wamishenari, hata katika makundi

yetu ya Kipentekoste. Mbona, baadhi ya makanisa yetu ya Kipentekoste, ama madhehebu ya Kipentekoste, hayana budi, wamishenari wetu, kabla hawajaondoka kwenda ng'ambo, inawabidi kusimama mbele ya wataalamu wa magonjwa ya akili na kufanyiwa uchunguzi wa akili. Hiyo ni kweli. Nimekuwa moja kwa moja shuleni wakati lilipofanywa. Inawabidi kusimama mbele ya uchunguzi wa akili, kumwacha daktari akwambie, na labda daktari huyo ni asiyeamini (Huh?), kusimama mbele ya da—daktari, m—mtaalamu wa magonjwa ya akili, apate uchunguzi wa akili.

115 Tunachohitaji leo si uchunguzi wa akili; uchunguzi wa akili ni kama tutaamini Neno la Mungu au la. Kama huliamini Neno la Mungu, basi una kasoro, hakika kabisa. Huenda ukawa na kila namna ya digrii, Ph.D., D.D.D., na L. maradufu D., chochote unachoweza kuwa nacho, bali kama huamini Neno la Mungu, wewe ni asiyeamini, kweli.

116 Loo, miaka kumi shuleni ili kujifunza kuwa mmishenari; miaka kumi, inawabidi kwenda shuleni kujifunza kuwa mmishenari. Loo, jamani, hilo ni baya sana. Miaka kumi kujua kama unaweza kujifunza lugha. Unafanya nini unapojaribu kuzungumza hiyo lugha? Unaiharibu kama Mjerumani fulani, amekuwa hapa majuma sita na kujaribu kuzungumza Kiingereza, hujui anachozungumzia, vivyo hivyo. Baadhi yao, hata hawana kitu cha kujifunzia. Utaijuaje hiyo lugha? Italeta faida gani, isipokuwa uwe na kitu cha kuwathibitishia baada ya kufika kule? Unakuwa tu mmoja wao, matatizo yale yale waliyo nayo, hivyo tu.

117 Hatuna haja ya kujifunza lugha, tunahitaji kujifunza lugha ya Kimbinguni inayoshushwa kutoka Mbinguni kwa nguvu za Roho Mtakatifu, lugha ya Injili: Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

118 Jinsi hawa walivyo tofauti siku hizi, na walivyokuwa kwenye Siku ya Pentekoste! Hawakuwafanyia uchunguzi wa kiakili, hawakuwapitisha shuleni, hakuna dalili ya wao kuwahi kuwa huko, lakini wao kwa-. . .haikuwabidi kungojea miaka kumi, walingojea siku kumi, nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu. Walikaa pale mpaka waliposhawishika ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ahadi.

119 Vipi kama wangalikuwa huko kwa siku saba? Huenda Andrea angemwambia Filipo, "Aisee, hivi hujui nini? Alitwambia tuje huku tungojee. Ninaamini tayari tumempata. Na tumkubali kwa imani." Vipi kama Petro angalimwambia Yohana, "Unajua nini? Alituambia tuje huku. Kwa hiyo sisi . . . mimi . . . tayari tumekuwa hapa siku tisa. Na—naamini inatupasa tu kulikubali, tuendelee na huduma yetu." Kama wangefanya hivyo, wasingekuwa na huduma.

120 Lakini Yeye alisema, “Nitatuma ile Ahadi.” Ahadi ni nini? Wangeweza kurudi katika—katika, katika Isaya 28:19, na kusema, “Amri lazima iwe juu ya amri; kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo, na pale kidogo. Shikilia yaliyo mema. Kwa kuwa kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa. Na hii ndiyo sabato niliyosema kwamba waisikie.” Hiyo ni kweli.

121 Yoeli alisema, katika 2:28: “Itakuwa katika siku za mwisho,” asema Mungu, “Nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; wana wenu na binti zenu watatabiri. Na juu ya wajakazi Wangu na mtumishi wa kike nitawamwagia Roho Yangu. Wazee wenu wataota ndoto, vijana wenu wataona maono.” Jinsi kutakuwako na nguzo za moto, na moshi na mvuke, yale mambo hayo yangefanya yapate kutimia, lakini, “kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.”

122 Walingojea mpaka Mungu aliposhusha nguvu za kusadikisha za ushahidi kwamba Roho Mtakatifu alikuwepo, Moto ulikaa juu ya kila mmoja wao, kama miale ya moto ikiwaka juu yao. Walipotoka nje mtaani, hata wasingeweza kuzungumza lugha yao wenyewe, ndipo wakanena katika lugha ya hao watu waliosimama huko nje wakiwasikiliza. Amina.

123 Walishawishika, na hiyo ndiyo sababu waliiteketeza dunia katika siku hiyo. Nayo Injili ikaenea kila mahali kwa sababu walikuwa wameshawishika kabisa kwamba ilikuwa ni Kristo aliyefufuka, kwa kuwa walimwona akifanya miujiza miongoni mwao kama alivyoahidi angefanya. Walishawishika kwa sababu Neno la Mungu lilidhihirishwa ndani yao. Ni tofauti jinsi gani leo na Wapentekoste!

124 Jinsi ilivyokuwa tofauti! Kamwe hawakuwapeleka mbele ya mtaalamu wa magonjwa ya akili, ama chochote kile, waone kama kweli wangeweza kustahimili jaribio la akili au la. Hawakufanya hivyo. Hili hapa jaribio la akili: angalia jinsi walivyo mbali na *Hili*. Naam. Naam. Baadhi ya watu hao hata hawakuwa na elimu ya kutosha kuandika jina lao. Hiyo ni kweli. Hata wasingeweza kuandika jina lao, bali walishawishika, kisha wakahusika.

125 Kama wangeshawishika na walikuwa na Mungu moyoni mwao, ingewabidi kuhusika, kwa kuwa Kristo alihusika sana na dhambi za ulimwengu, hata akautoa Uhai Wake kwa ajili yake. Na kama Kristo yuyo huyo alikuwa ndani yako, halafu umeshawishika ya kwamba ni Kristo, utahusika pia. Hiyo ni kweli. Hatuhusiki kuhusu kuipeleka Injili.

126 Mhudumu fulani, labda Bwana alimwita mahali padogo ambapo anaweza kuhubiri, ama kufanya kazi fulani kwa ajili ya Bwana, kama hawamlipi tu, vema, mtu fulani ampe malipo bora zaidi *kule*, kwa sababu ya pesa ataondoka *hapa* ambapo

Mungu alimtuma, na kwenda *kule* ambako kuna pesa nyingi zaidi, hajashawishika bado ilikuwa ni Mungu aliyemwita pale.

127 Kama umeshawishika kabisa, kama inakubidi kula ugali wa mahindi na kunywa maji ya chumvi, hujali nini, huyo mhubiri mwingine anaweza kula, milo mitatu ya kuku kwa siku na kuendesha Kadilaki iliyoyoyozwa, hujali, kwa kuwa kama umeshawishika kwamba ni uweza wa Mungu uletao wokovu, nawe umeitwa kwa huyo Roho, aliyemfufua Yesu katika wafu, nawe unamwona Yeye akitenda kazi pamoja nawe, basi unahusika kuhusu wokovu wa ndugu yako. Sio, kumpa mkono, kuandika jina lake kwenye kitabu, hana budi kuzaliwa mara ya pili na Roho wa Mungu, hana budi kuwa na nguvu za Kristo maishani mwake zinazombadilisha kutoka mtu aliyekufa akawa kiumbe hai, jiwe hai, lililoinuliwa, na warithi pamoja na Kristo katika Ufalme, walioketi katika ulimwengu wa Roho. Huna budi kushawishika kwanza.

128 Kamwe usingeweza kuja kwenye mkutano, ungeufanyia mzaha mkutano ambapo Roho Mtakatifu alikuwa akishuka, ungefanya hivyo mpaka ushawishike. Ndipo basi unaposhawishika, basi unahusika. Lakini sasa, ngoja mpaka utakaposhawishika, ndipo utahusika.

129 Hawakungojea elimu, hawakungojea mpaka wawe na shule kubwa, hawakungojea mpaka uwape makaratasi fulani, hawakungojea mambo haya, walikuwa Naye, Hilo tu ndilo walilohitaji. Nao wale watu waliokuwa wakiwaendea, walishawishika kabisa kwamba Hilo ndilo tu watu walilohitaji, nami ningali nimeshawishika na jambo lile lile.

130 Hatuhitaji upuuzi huu wote hapa ambao *unaitwa* Ukristo siku hizi, kutembea pamoja, na kujaribu kuungana pamoja, kama Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Nini katika ulimwengu? Wakati kutokuamini, na wasioamini, na kila kitu kikichanganyikana pamoja, tunaendeleaje kamwe? Tunachohitaji ni dini ya mtindo wa kale, ya huko nyuma msituni, ya anga la bluu, inayoua dhambi. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Nguvu za injili, na Roho Mtakatifu akihubiriwa katika nguvu za ufufuo. Pata ufufuo mzuri wa Mtakatifu Paulo na Roho Mtakatifu wa Biblia, akiwashawishi watu. Tunahitaji kumwona Kristo akija miongoni mwetu na kutenda, na kufanya mahali hasa aliposema, "Ye—yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya, nyingi kuliko hizi atafanya, maana mimi naenda kwa Baba Yangu."

131 Yuko wapi daktari hapa nyuma, ambapo ilinukuliwa muda mfupi uliopita, "Mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata mwisho wa dunia"? Nami nimeshawishika Yeye yupo hapa, Yeye alisema atakuwa hapa, "Walipo wawili au zaidi wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao." Hivyo sivyo ilivyo, basi

hayo mengine sivyo yalivyo; Yote ni sawa, ama Yote ni uongo. Ninaamini ni, kila Neno, ni kweli.

132 Ninaamini Yeye yupo hapa sasa, ninaamini Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste yuko Chicago, usiku wa leo. Ninashikilia sehemu Yake moyoni mwangu, nami nimeshawishika ya kwamba ni Roho Mtakatifu yeye yule, mambo yaya haya. Hilo linanifanya nihusike kuhusu kupeleka Ujumbe huu kwa ndugu au dada yangu mahali fulani, ndugu yangu Mbaptisti, ndugu yangu Mmethodisti, ndugu yangu Mkatoliki, popote walipo.

133 Nimeshawishika ya kwamba Huyu ni Mungu, nami nimeshawishika ya kwamba Yesu yuaja, nimeshawishika ya kwamba huku ndiko kuonekana Kwake mara ya kwanza katika mfano wa Roho Mtakatifu katika siku za mwisho, kwa sababu nabii alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Nimeshawishika ya kwamba Maandiko yametimia. Ninashawi-. . . Nimeshawishika kwamba ulimwengu uko kwenye kilele cha maangamizi, utaratibu wa ulimwengu, kosmos, lakini, ninaamini, nimeshawishika ya kwamba kuja kwa Bwana kumekaribia, nimeshawishika kwamba Kile tulicho nacho ni Roho Mtakatifu.

134 Nimeshawishika ya kwamba Chicago imetikiswa, si chakula cha mzinga hapa nje, majengo haya, na huku na huku mtaani, wanawake hawa waliovalia kizinifu, na wanaume hawa wanaofanya yasiyofaa, walevi, na kufanya yasiyofaa, mimi . . . kwenda kanisani, na kula maskini mkate mwepesi, mkate wa boflo, kufanya mkate mwembamba kutokana nao, siamini katika upuuzi huo, wakipiga mbweu, wiski na kadhalika pumzini mwao, kisha wanatoka wanaenda kula ushirika, jina lao likiwa kwenye kitabu fulani cha kanisa, na kujiita wenyewe Mkristo, siamini hilo.

135 Ninaamini Kanisa la Yesu Kristo ni Kundi lile lililoitwa litoke ambalo limetakaswa kwa Damu ya Yesu Kristo, na kutengwa kwa ajili ya utumishi. Nami ninaamini jambo hili tunaloona likitendeka ni kule kuonekana kwa Bwana Yesu miongoni mwetu, kama Yeye alivyosema.

136 Kumbukeni, katika siku za Sodoma huyo alikuwa ni Mtu aliyesimama pale ambaye angeweza kula na kunywa, bali ilikuwa ni Mungu katika huyo Mtu, ikionyesha ya kwamba Mungu angeonekana katika siku za mwisho katika umbo la mwili wa mwanadamu katika Kanisa Lake, ambaye ni Bibi-arusi Wake, Nao wangefanya mambo yale yale aliyofanya. Amina. Ninaamini hilo.

Mtu fulani alisema, "Una kichaa, Mhubiri."

"Vema," nikasema, "niache basi, nina furaha zaidi hivi kuliko nilivyokuwa vinginevyo." Vema.

137 Walishawishika! Walishawishika ya kwamba yote waliyohitaji ilikuwa ni Yesu, nao walishawishika ya kwamba yote watu waliyohitaji ilikuwa ni Yesu.

138 Tunafanya nini Afrika? Huyu hapa Mwafrikana ameketi *hapa*. Tunaenda kule na kuwafundisha hao jamaa kusoma, kuandika, na hesabu. Tunafanya nini? Kuwatuma kule chini, nao wanafanyika nini? Mtoto wa kuzimu maradufu zaidi ya walivyokuwa hapo mwanzo. Wana dhambi zao za kikabila, na wanapoingia, wanachukua dhambi za mzungu. Hiyo ni kweli. Inamfanya mbaya zaidi kuliko alivyowahi kuwa, huko nje uani, na kadhalika. Hiyo ni kweli.

139 Mbona, yeye ni mwuaji, anakuwa mbakaji, yeye ni kila kitu kingine. Anakunywa wiski ya mzungu, anachukua dhambi zake mwenyewe. Wakati akiwa huko nje katika kabila, kama angefanya jambo kama hilo, angeuawa kwa ajili yake. Hiyo ni kweli. Mbona, yeye hahitaji elimu, anahitaji wokovu, anahitaji nguvu za ufufuo kuubadilisha moyo huo, hilo humfanyia jambo fulani. Amina. Hmm! Hiyo ni kweli.

140 Naam, bwana. Alishawishika ya kwamba Hilo ndilo tu walilohitaji, nao walimhitaji tu Yeye, nao walijua ya kwamba Yeye angetimiza mahitaji yao yote. Haikuwalazimu kuwa na kadi ya utambulisho, haikuwalazimu kuwa na madhehebu nyuma yao, walikuwa na Yesu, Naye alitimiza yote waliyohitaji.

141 Nafikiri ya kwamba kanisa linapaswa kusahau mengi ya upuuzi huu hapa, wakati uamsho unapokuja mjini, "Hati gani za utambulisho? Ni nani anayeweza kukuunga mkono?" Kristo ndiye Msaada wetu, Kristo ndiye Shahidi wetu, sisi ni mashahidi Wake, hilo tu ndilo Chicago inalohitaji, si ushirikiano mkubwa na kitu fulani, wanahitaji nguvu za Kristo, utambulisho wa Roho Mtakatifu kuibadilisha mioyo ya watu, kuwafanya viumbe vipya. Kushawishika, kisha wanahusika.

142 Hebu tuone, wengine, yote waliyohitaji ilikuwa ni Kristo, Huyo ndiye yote wanayohitaji siku hizi. Haikubidi kungojea, na kwenda shuleni, na kuchukua miaka thelathini na mitano kabla hujapata kamwe, umezeeka mno, ni vigumu, basi kwenda huku na huku. Utafanya nini? Hubiri Injili. Naam, bwana. Si elimu, msitoke mwende mkawaelimishe, tokeni mwende mkawaokoe, Yesu alisema. Hiyo ni kweli.

143 Kama vile Hudson Taylor, yule mmishenari mashuhuri, wengi wenu mnajua, wa Uchina, kulikuwa na mvulana wa Kihindi, ama, sivyo, mvulana wa Kichina siku moja aliamka, akaokoka, ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yake, akamwendea Bw. Taylor, naye akasema, "Bw. Taylor, nifanye nini? Niingie shule gani? Nifanye nini?" Kisha kasema, "Je, nichukue miaka hii ya masomo ambayo kanisa linahitaji?" na kadhalika.

144 Bw. Taylor akasema, “Usichukue mshumaa wako na kuuchoma nusu kabla hujaona kama unawaka au la.” Akasema, “Nenda mara unapowashwa mara ya kwanza.”

145 Loo, nitasema jambo lile lile. Huna haja ya kungoja na kuiona ikijaribiwa, na kujaribiwa, na kujaribiwa, na kuchukua majaribu mengi, na dhiki, na masomo haya yote, na kupata Shahada yako ya Sanaa, na Ph. na D.D. yako, na kadhalika namna hiyo. Kama huna hizo zote, hilo ni sawa, bali kama huna hizo, nenda wakati—wakati umewashwa. Kama huwezi kufanya zaidi ya kuwaambia uliwashwa, waambie jinsi ulivyowashwa. Hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya, kwa vyovyote vile.

146 Mungu aliuwasha maskini mshumaa wako, nenda ukawaambie jinsi ulivyowashwa. Amina. Achana nao, waambie tu jinsi mshumaa ulivyowashwa. Hebu wao. . . Ndipo Mungu atashughulikia yaliyosalia. Jambo ni kwamba, ni kuuwasha mshumaa huo kwa Moto kutoka madhabahuni naye Mungu anauidhinisha kwa nguvu za Roho Mtakatifu, na kufufuka kwake Kristo.

147 Achaneni nao, msiwaelimishe, msijaribu kuwafundisha vitu hivi vyote ndani yao. Mnaona kile kilichotufanya: kundi la makafiri wajinga. Hiyo ni kweli, wakikana Neno la Mungu kwa mfano wa utauwa, ingekuwa afadhali kutosikia habari Zake hata kidogo. Hiyo ni kweli.

148 Tunachohitaji ni kuwashwa kwa mishumaa, tunachohitaji ni maisha yaliyowashwa, yanayowaka moto kwa nguvu na ufufuo wa Kristo, yakiangaza Nuru ya namna ile ile aliyotoa Yeye. Ninaamini hilo.

149 Usingoje mpaka umeungua nusu, ukijaribu kujifunza lugha fulani, ama kupata kibali cha shirika fulani, wakati Yeye anapokuwasha, shika njia. Amina. Waambie tu ni tukio la namna gani ulilokuwa nalo ulipowashwa, ndipo labda watawashwa, wawashwe na Nuru yako. Naam, bwana.

150 Yule kipofu aliyezaliwa kipofu, yeye ni mfano mzuri kwetu sote. Sasa, yeye alizaliwa kipofu, Yesu alikuja na kumfanya, akayafungua macho yake. Nao hawa hapa madaktari wote wa falsafa wanakuja, na—na madaktari wote, na makuhani, na, wa hekalu wakaja, na Mafarisayo, nao walikuwa wakijaribu kubishania theolojia naye.

151 Sasa, yeye—yeye asingeweza kubishania theolojia, hakujua lolote kuihusu, lakini, ndugu, alikuwa na jambo moja: alilokuwa na ujuzi wake. Jaribu kubishania hilo naye, jaribu kumwambia asingeweza kuona, angekuonyesha upesi sana anaweza kuona. Hiyo ni kweli. Huenda asielewe ma—mabishano yote waliyopaswa kutoa, lakini hakika aliwakomesha aliposema, “Ni ajabu kwamba Mtu huyu anaweza kuyafungua macho ya kipofu, na hata hivyo, mnadai kuwa jinsi mlivyo, wala hamjui lolote kumhusu.” Ninaamini alikuwa na akili timamu, kama

hakuwa na theolojia nyingi iliyookwa ndani yake, ama chochote kile, hakika alikuwa nayo.

Akasema—akasema, "Vema, mtu huyu ni mwenye dhambi."

Akasema, "Kama Yeye ni mwenye dhambi au la, sijui, lakini jambo hili moja najua: ambapo nilikuwa kipofu, sasa ninaweza kuona."

152 Vema, mnaweza kusema nina kichaa mkitaka, mnaweza kusema niko nje ya mapenzi ya Bwana mkitaka, ila jambo moja tu: Ambapo wakati mmoja nilikuwa mwenye dhambi, nimeokoka, ambapo wakati mmoja nilikuwa nimekumbwa na huzuni na kuondoka, nina furaha katika Bwana Yesu, ninajua kuna jambo fulani lililonipata.

153 Kama vile dada mmoja mweusi alivyosema wakati mmoja mkutanoni, alisema, "Ninataka ninyi nyote mjue jambo moja," kasema, "Siko jinsi ninavyotaka kuwa, na siko vile ninavyopaswa kuwa, lakini kuna jambo moja hakika, siko jinsi nilivyokuwa." Nawaambia, hilo ni jambo zuri.

154 Unajua ulipopita kutoka mautini kuingia Uzimani, wakati Mungu anapokushika na kubadilisha maisha yako, hubadilisha. . .?. . .na kubadilisha kila kitu kilicho ndani yako, na kukufanya kiumbe kipya. Amina. Hiyo ndiyo tunayohitaji, mishumaa iliyowashwa. Naam, bwana.

155 Naam, angeweza kuona, hilo ni jambo moja, usingeweza kubishania jambo hilo naye, hu—huenda ulimwambia jambo moja au lingine. Huenda hakuelewa mafundisho yote ya hekalu, na kadhalika, bali alikuwa na u—ushuhuda mzuri, tukio zuri, zaidi ya vile wangeweza kutoa. Pamoja na theolojia yao yote, hata hivyo, wasingeweza kutoa kisa kimoja wakati wowote, mtu aliyezaliwa kipofu, angepata kamwe kuona. Kwa hiyo wasingeweza kubishania hilo kabisa, kwa hiyo iliwabidi kumwacha aendelee, kwa hiyo walimnyakua tu, na kumtupa nje ya jengo.

156 Huo ulikuwa ndio msimamo wao wakati huo, ni jambo lile lile leo, wao ni. . .?. . .Lakini bado kuna: "Wakati mmoja nilikuwa kipofu, na sasa naona." Amina.

> Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika tamu,
> Iliokoa mwovu kama mimi!
> Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, na sasa nimepatikana,
> Nilikuwa kipofu, lakini sasa ninaona.
>
> Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu kuogopa,
> Na neema ikaniondolea hofu zangu;
> Jinsi neema hiyo ilivyoonekana yenye furaha
> Saa ile niliyoamini kwanza!

Loo, jamani! Hiyo na iwe hadithi yangu.

157 Papa hapa Chicago, Dwight Moody, yule mwinjilisti mashuhuri ambaye kweli alikuwa na uamsho mkuu hapa, wakati mmoja huko Chicago, mwajua, yeye alikuwa ni mtu asiye na elimu. Hawakuninii . . . Walimchukia pia, mbona, hakika, walimchukia.

158 Hakuwa na elimu hata kidogo, naye akaenda London, Uingereza, akazungumze na wakukni ambao, loo, jamani, kila kitu hakina budi kuwa *hivi-na-hivi*. Naye Bw. Moody, akisimama mbele ya maelfu yao usiku mmoja, alianza kusoma Biblia, naye alikuwa amejizoeza neno fulani kujaribu kulitamka vizuri, naye akalitamka vibaya. Akasugua kichwa chake akaanza tena, akajaribu tena, na kulitamka vibaya tena. Akaangalia kule, na hao jamaa wote, mwajua, walikuwa karibu tu kuangua kicheko kikubwa. Akajaribu tena, akalikosa tena, akaifunga Biblia, na kuangalia juu kuelekea Mbinguni, kasema, "Mungu, sijui maana yake, lakini Wewe unifunulie."

159 Ndugu, alipata kitu fulani, ambacho aliitikisa nchi nzima kwacho. Naam, bwana. Huenda hakuwa, hakulitamka hilo Neno, bali Mungu alimpa nguvu ambazo hilo Neno lilimaanisha. Afadhali niwe na hizo kwa vyovyote vile, wakati wowote. Naam. Mungu alimpa kitu kilichoitikisa Uingereza. Hiyo ni kweli. Tunahitaji baadhi ya hizo, usiku wa leo, ambazo alikuwa nazo wakati huo. Asingeweza kutamka maneno yake vizuri, bali yeye—yeye hakika alikuwa na ninii—ninii—ninii . . . Mungu Ambaye alikuwa amesema hilo Neno alijitokeza jukwaani, aliyeliandika Neno. Naam, bwana.

160 Sasa, kama vile maskini Buddy Robinson, na wengi wenu mnamkumbuka, mbona, alikuwa—aliwajali sana watu. Kwa nini? Alishawishika. Nilikuwa nikisoma juu ya Uncle Buddy, tulimwita Uncle Buddy, yule nguzo ya kale ya kanisa la Nazarayo, nilikuwa nikisoma kitabu chake hapa si muda mrefu uliopita, alikuwa na maskini nyumbu, alikuwa akimwita Ellie. Naye alikuwa, akajizoeza, alitaka kufanya mazoezi ya utakaso, naye aliamini ya kwamba tunapaswa kujiepusha na dhambi. Basi alisema alikuwa akilima mahindi yake, wala asingeweza kumfanya Ellie atembee kwenye mstari ulionyooka, basi akamkasirikia Ellie, kwa sababu hangefuata mstari ulionyooka, ndipo akakuta kwamba Buddy hakuwa akitembea kwenye mstari ulionyooka pia.

161 Kwa hiyo basi, alikuja kugundua kwamba alikanyaga mahindi yake, naye akamkasirikia sana maskini huyo nyumbu hata akamshtua-shtua huku na huku, yapata mara chache, kisha hasira yake ikapanda, akakimbia huko nje na kumwuma masikioni kwa nguvu alivyoweza. Maskini huyo nyumbu akakimbia kidogo kisha akasimama, akaenda kule, na kuketi juu ya lundo dogo la mawe.

162 Akasema aliketi pale na kuwazia, "Hivi mimi si tamasha?

Huku nje nikihubiri utakaso huku nywele za nyumbu zikiwa kwenye meno yangu kutokana na kuuma sikio la nyumbu." Mnajua, Uncle Buddy alikuwa na ucheshi. Akasema, "Ellie?" Kasema aliyafingirisha macho yake makubwa, ya hudhurungi kote, kasema, "Samahani nilifanya hivyo. Nisamehe."

163 Kasema, "Maskini Ellie akaniangalia kana kwamba kusema, 'La, sitakusamehe, maana usipopata dini zaidi ya uliyo nayo sasa, utanifanyia hivyo tena.'" Kwa hiyo, hivyo karibu ndivyo ilivyo. Hakuna haja ya kujiunga naye, afadhali tu ukae mbali...?...

164 Asingeweza kuzungumza vizuri sana, hotuba yake ilikuwa mbaya, lakini, ndugu, alishawishika ya kwamba Yesu Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu, yeye, alishawishika ya kwamba aliteswa nje ya malango apate kuwatakasa watu kwa Damu Yake Mwenyewe, naye alihusika kuhusu watu katika siku zake, maana alikuwa ameshawishika. Naam, bwana.

165 Kwanza, huna budi kushawishika kabla ya kuweza kuhusika. Hivi huamini hilo? Naam, bwana.

166 Wakati mmoja, tukiwa na uamsho nchini, kulikuwa na jamaa wa mashambani aliyeingia, amevaa ovaroli, nikafanya wito wa madhabahuni usiku mmoja, naye akaja madhabahuni, akainama, akasema, "Unamaanisha kwamba huyu Roho Mtakatifu ni kwa ajili yangu?"

"Naam, Bwana."

Akasema, "Nitampataje?"

Nikasema, "Jinsi tu Biblia inavyosema umpate."

167 Na kwa hiyo akasema, "Vema, mimi hapa ninakuja," akasema, "Ninamtaka." Akashuka pale na kuomba kidogo, akaangalia juu tena, kasema, "Siendi popote."

Nikasema, "Wewe ndiwe chanzo cha hilo, si ahadi ya Mungu."

Naye akashuka pale na kuomba, yapata saa nane usiku huyu hapa anakuja, alikuwa Naye, alibadilika.

168 Sasa, hakuwa na elimu yoyote, hakuwa na kitu ila gari la kale la Ford na tukio. Lakini nitawaambia yale aliyofanya, alishawishika kwamba ilikuwa ni Mungu, alihusika kuhusu jamii yake. Naye maskini mvulana huyo mwenye tukio hilo na gari la Ford aliwaokoa watu wengine ishirini wakati wa ule uamsho. Yote aliyokuwa nayo yalikuwa ni tukio na lori la Ford, naye alikuwa ameshawishika kwamba lilikuwa sahihi. Tuna zaidi ya hayo usiku wa leo, sijui kama tunaweza kuhusika nayo, kama tu vile yule mkulima alivyokuwa, ameshawishika.

169 Samsoni, loo, hakika, Samsoni siku moja, alishawishika ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu, alishawishika ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye wakati angeweza kushikilia

vishungi vyake saba huko nyuma, na alijua ilikuwa ni ahadi aliyopewa na Mungu, alihusika kuhusu watu wake, hakuwa na kitu cha kupigana nacho ila mfupa wa taya la nyumbu, bali aliwaua Wafilisti elfu moja. Kwa nini? Alishawishika, ndipo basi akahusika.

170 Daudi, akiwa na kombeo, lakini shida ilikuwa nini? Alishawishika ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu, alihusika kuhusu kondoo wa baba yake, naye hakuwa na mengi sana ya kupigana nayo, bali alishawishika kisha akahusika, kwa hiyo akamfuatilia kondoo wa baba yake, na akamrudisha. Naam, bwana.

171 Sasa, tungeweza kukaa hapa kwa saa moja ama zaidi, bali hatutafanya hivyo. Ninataka kusema jambo moja: Vipi kuhusu Ndugu Boze hapa? Yeye hadhaminiwi, hiyo ni kweli, hajadhaminiwa, hajafadhiliwa na mtu yeyote, bali ameshawishika ya kwamba watu hao wanahitaji Injili, naye anahusika nayo, kwa hiyo anajaribu kuwapelekea Injili. Nafikiri kama yeye anahusika, tunapaswa kuhusika, pia. Hivi hamwoni hivyo?

172 Kama ameshawishika ya kwamba wanaihitaji, nasi sote tumeshawishika, ndugu daktari aliyekuja hapa ameshawishika, hawa wamishenari wengine wameshawishika, basi kama tumeshawishika, tunapaswa kuhusika. Hivi hamwoni hivyo? Tunapaswa kuhusika.

Mnasema, "Vema, hiyo ni sehemu gani kwangu?"

173 Inanikumbusha juu ya katuni ndogo niliyoona si muda mrefu uliopita kwenye gazeti. Katika kufunga huenda nikasema hivi: Katuni hiyo ndani ya gazeti, nyumbani kwetu ni upande wa pili wa mto, Courier Journal, na kulikuwa na pi—picha ya baba na mama, walikuwa nje wakinywa pombe usiku kucha, ndipo Jumapili asubuhi, ilikuwa yapata saa tatu, nao walikuwa na picha za Kristo kote nyumbani, na Biblia kwenye mtoto wa meza, na—na kote mahali walipokuwa wamelala pale wakilala usiku kucha, sigara sakafuni, na kadhalika, na chupa zimewekwa, mvulana mdogo alikuwa ameamka, akanawa uso wake, akala kiamshakinywa chake, na kujiandaa, akibisha mlangoni, kasema, "Ni nani kati yenu nyote, atakayenipeleka kwenye shule ya Jumapili?" Hiyo ni kweli, hakuna mtu anayehusika.

174 Nafikiri tunapaswa kuhusika. Nafikiri tunapaswa kumsaidia Ndugu Boze, na mmishenari mwingine yeyote kwa yote tuliyo nayo. Jambo la kwanza tunalopaswa kufanya ni kushawishika ya kwamba Yesu yuaja, huu ndio mpango Wake, tunapaswa kumjali ndugu yetu, kama yeye ni mweusi, manjano, hudhurungi, ama mweupe, tunapaswa kuhusika kuhusu hao watu kule. Na kama hatuwezi kwenda, tunapaswa kuchimba

chini, na kufanya yote tuwezayo kuwaunga mkono wale ambao Mungu amewaita waende.

175 Na tuinamishe vichwa vyetu.

> Wakati kaa la moto lilipomgusa nabii,
> Likimfanya safi awezavyo kuwa,
> Wakati Sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"
> Ndipo akajibu, "Bwana, hapa, nitume mimi."
>
> Nena, Bwana wangu, loo, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu upesi;
> Nena, Bwana wangu, nena, nanii wangu . . .
> Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi." (Angalien mjini, yatazameni mataifa.)
>
> Mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na aibu,
> Sikiliza kilio chao cha huzuni na uchungu;
> Hima, ndugu, hima kuwaokoa;
> Jibu upesi, "Bwana, hapa . . ." (Kama huwezi kwenda, mtume mtu mwingine.)
>
> Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu upesi;
> Nena, Bwana wangu, loo, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nena, Bwana Wangu*—Mh.]

> "Nani ataenda na kufanya kazi kwa . . ."

176 Kumbuka tu sasa, wakati muziki unapopigwa, nawe unavumisha, je, umeshawishika? Je, umeshawishika ya kwamba Mungu yupo hapa? Je, unaweza, umeshawishika ya kwamba Huyu ni Roho Mtakatifu? Je, unahusika? Wangalie mamilioni, dhambi na aibu wanakufa.

> Loo, nena, Bwana wangu, (Unataka nifanye nini, Bwana?), nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu upesi;
> Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."

177 Baba wa Mbinguni, tunawazia juu ya Isaya, ambaye huyu mshairi alimwandikia wimbo huu mzuri. Alikuwa ameegemea begani mwa mfalme mzuri kwa muda mrefu, lakini Mungu akaondoa msaada kutoka chini yake, ndipo akaenda madhabahuni. Mungu, wakati mwingine inakubidi kuondoa msaada kutoka chini yetu, unaacha ulimwengu utukatae, wakati mwingine marafiki zetu, ndipo tunapiga magoti.

178 Ndipo akawaona Makerubi wakiruka jengoni, akaona alikuwa akiishi miongoni mwa watu wachafu, wenye midomo michafu, hakuliona mpaka Mungu aliponena. Ee Mungu, linene!

. . . Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."

179 Baba, tunajiweka wakfu Kwako, usiku wa leo, katika ibada. Tu—tunaita kwa uaminifu, kwa mioyo yetu yote, Sauti ya Mungu inene nasi. Tujaribu sasa, Bwana, tusafishe, jalia tupitie toharani, sasa hivi, ambapo tunaweza kuzitakasa nafsi zetu na kutokuamini, kujitenga na kanuni za imani na mitindo ya ulimwengu huu.

180 Tunatambua hatuna muda mrefu zaidi wa kwenda, liko mlangoni. Tunaona Israeli ta—taifa, tunaona, kama ilivyokuwa katika siku za Israeli, sambamba sana na taifa hili, jinsi ambavyo waliingia, na kuichukua nchi kutoka kwa watu wengine, wakawafukuza wenyeji, kama tulivyofanya. Tunaona walikuwa na watu mashuhuri hapo mwanzo, walikuwa na Yoshua, kisha walikuwa na Daudi, kisha walikuwa na Sulemani, lakini hatimaye wakawa na Ahabu pamoja na Yezebeli kumtawala.

181 Baba, tulikuwa na Washington na Lincoln, lakini sijui tunaelekea wapi. Ee Mungu, tunamhitaji Eliya leo!

Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utasema nasi upesi. Ibariki mioyo yetu pamoja, tufasirie mapenzi Yako, Bwana, tupate kujua la kufanya.

182 Wabariki wahudumu hawa hapa, Bwana, wengi wao wanatoka kwenye matabaka mbalimbali, mashirika mbalimbali, madhehebu. Mungu, watakaporudi kule nyuma, wao, jalia wawe nu—nuru isiyoweza kuzimwa, wala haiwezi kufichwa chini ya kanuni fulani ya imani, bali jalia waiangaze Nuru ya Mungu ambayo imewashwa mioyoni mwao na Roho Mtakatifu.

183 Mbariki kila mmoja, tunakungojea Wewe. Mbariki maskini ndugu yetu wa thamani na mpendwa. Ninaweza kuwazia juu ya yapata miaka mitatu iliyopita, akiketi hapa kwenye rasi hii, maskini mikono yake imenikumbatia akilia, Nawe ukanena nasi pale, Bwana. Na sasa hawezi kuridhika hapa tena, hana budi kuondoka. Mungu, kuwa pamoja naye, kuwa pamoja na Ndugu Joseph, mlinde na umbariki, mpe nafsi nyingi, Bwana.

184 Mungu, wabariki vijana hao. Ninapowaona wakiendesha baiskeli hizo, baadhi yao, Bwana, huko nje bila hata viatu miguuni mwao, ndipo tunafikiri tunajitolea. Mioyo yao inawaka kwa ajili ya watu wao, kwa sababu wameshawishika na wanahusika.

185 Mungu, tusaidie sote kuhusika pamoja, kuuona Ufalme wa Mungu ukija. Na jalia tuendelee kuamini yale Yesu aliyotwambia, ya kwamba aliomba kwamba sote tupate kuwa mmoja katika Yeye. Bariki jitihada zetu katika kujaribu kutimiza maombi haya. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

186 Samahani kuwashikilia kwa muda mrefu sana. Mungu awabariki.

Vema, Ndugu Boze.

62-0521 Kushawishika Na Kisha Kuhusika
Stephen Mather High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org